



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI  
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI



JIMBO LA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI

Kumb. Na. MZA/MDC/E/200/08/2

Tarehe 22.08.2023

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA**

Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo la Misungwi kwa kuzingatia kanuni ya 12 na 13 za Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, anakaribisha maombi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi za watendaji wa vituo vya kupigia kura kwa ajili ya uchaguzi mdogo utakaofanyika tarehe 19 Septemba, 2023 katika Kata ya Mwaniko kama ifuatavyo: -

1. Msimamizi wa Kituo cha Kupigia Kura (Nafasi 13).
2. Msimamizi Msaidizi wa Kituo cha Kupigia Kura (Nafasi 26).
3. Karani Mwongozaji Wapiga Kura (Nafasi 13).

**A. SIFA ZA WAOMBAJI WA NAFASI YA MSIMAMIZI AU MSIMAMIZI MSAIDIZI WA KITUO CHA KUPIGIA KURA**

- (a) Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi;
- (b) Asiwe shabiki au kiongozi wa chama cha siasa;
- (c) Awe mwadilifu, mtiifu na mwenye akili timamu;
- (d) Awe amemaliza elimu ya kidato cha nne (4) au zaidi na anaweza kusoma na kuandika vizuri. Pia, anayeweza kusoma na kuelewa kitabu cha Maelekezo ya Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura; na
- (e) Ikiwezekana awe mkazi wa kata ambayo anaomba kufanya kazi.

**B. SIFA ZA WAOMBAJI WA NAFASI YA KARANI MWONGOZAJI WA WAPIGA KURA**

- (a) Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi;
- (b) Awe mkazi wa kata ambayo atafanyia kazi ya kuongoza wapiga kura;
- (c) Ikiwezekana awe mpiga kura wa kituo atakachofanyia kazi;
- (d) Awe mwadilifu, mtiifu na mwenye akili timamu;

- (e) Awe na elimu isiyopungua kidato cha nne na anayeweza kusoma na kuelewa kitabu cha Maelekezo kwa Makarani Waongozaji Wapiga Kura; na
- (f) Asiwe shabiki au kiongozi wa chama cha siasa.

**C. MALIPO**

Malipo yatakuwa kama ifuatavyo: -

- i. Siku ya Uchaguzi Msimamizi wa Kituo atalipwa posho ya Shilingi 60,000 kwa siku kwa muda wa siku mbili, posho ya chakula Shilingi 10,000 kwa siku moja na nauli Shilingi 20,000.
- ii. Msimamizi Msaidizi wa Kituo atalipwa posho ya Shilingi 50,000 kwa siku kwa muda wa siku mbili, posho ya chakula Shilingi 10,000 kwa siku moja na nauli Shilingi 20,000;
- iii. Karani Mwongozaji Wapiga Kura atalipwa posho ya Shilingi 50,000 kwa siku moja na posho ya chakula Shilingi 10,000.
- iv. Wakati wa mafunzo watendaji wote watalipwa posho ya Shilingi 50,000 na nauli Shilingi 20,000 kwa kila siku ya mafunzo. Mafunzo kwa wasimamizi wa vituo na wasimamizi wasaidizi wa vituo yatafanyika kwa muda wa siku mbili, na mafunzo ya makarani waongozaji wapiga kura yatafanyika kwa muda wa siku moja.

**D. MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE**

- i. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) wawili.
- ii. Maombi yote yaambatishwe na vyeti vya taaluma, nakala ya vyeti vya kidato cha nne, kidato cha sita au kuhitimu mafunzo kwa kuzingatia sifa alizonazo kwa mujibu wa Tangazo hili.
- iii. Waombaji waambatishe picha mbili zenye ukubwa sawa na picha iliyopo kwenye pasi ya kusafiria (Passport size) za hivi karibuni.
- iv. Waombaji ambao ni Watumishi wa Umma wapitishwe barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa waajiri wao.
- v. Waombaji watakaowasilisha taarifa na sifa za kugushi watachukuliwa hatua za kisheria endapo watabainika.


**Mwisho wa kutuma na kupokea maombi ya kazi ni tarehe 28 Agosti, 2023.**

**Anuani ya kutuma maombi ya kazi ni: -**




Msimamizi wa Uchaguzi,  
Jimbo la Misungwi  
S. L. P 20.  
Misungwi.

Limetolewa na:-



JOSEPH C. MAFURU  
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI  
JIMBO LA MISUNGWI

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI  
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI  
JIMBO LA MISUNGWI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI



TANZANIA